

# Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere

1. **Dakika 15 kabla ya miadi yako ya tiba ya mtandaoni, bofya kiungo ulichotumiwa kwenye barua pepe au ujumbe wa maandishi.**
   - **Usishiriki kiungo na wengine. Mtu 1 tu ndiye anayeweza kutumia kiungo hiki.**
     - **Ikiwa wengine wanahitaji kujiunga kwenye ziara, mwambie mtoa huduma pindi ziara inapoanza.**




2. **KidCare Anywhere itafunguka katika kivinjari cha intaneti kwenye simu yako.**
   - **Kivinjari cha intaneti cha Safari au Google Chrome kinapendekezwa.**

3. **Bofya Continue (Endelea).**





Ilisasishwa: Tarehe 4 Juni, 2025

4. **KidCare Anywhere hujaribu muunganisho wa intaneti, maikrofoni na kamera yako kabla hujajiunga kwenye ziara.**

    - **Bofya Allow (Ruhusu) kwa KidCare Anywhere ili kutumia maikrofoni na kamera yako.**





    - **Ikiwa kamera yako inafanya kazi, unaweza kujiona kwenye skrini wakati wa jaribio. Bofya Proceed (Endelea) wakati jaribio limekamilika.**




5. **Unawekwa kwenye chumba cha kusubiri cha mtandaoni. Mtoa huduma atajiunga kwneye ziara baada ya kukagua taarifa zako.**

    - **Usiache wala kupunguza skrini ya KidCare Anywhere ili kutumia programu au kupokea simu au kujibu ujumbe wa maandishi.**



# Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere


## Maagizo ya In-Call (Ziara kwa Mhudumu)

- **Kamera na Maikrofoni**
  - **Hakikisha kuwa camera (kamera) na microphone (maikrofoni) yako zimewashwa. Bofya kitufe iliuwashe au uzime.**

    - **ON (IMEWASHWA)**

    - **OFF (IMEZIMWA)**


      
      

  - **Ili kubadilisha kamera au maikrofoni yako:**


    1. **Bofya kitufe cha gia kilicho upande wa skrini wakati wa ziara.**

    2. **Tumia menyu kunjuzi ya Kamera au Maikrofoni kuteua kile unachotaka kutumia.**

- **Gumzo**
  - **Unaweza kutuma ujumbe wa gumzo kwa mtoa huduma wako wakati wa ziara.**
  - **Bofya kitufe cha Chat (Gumzo) ili ufungue gumzo. Andika ujumbe wako na ubofye Send (Tuma).**



- **Kuhitimisha ziara**
  - **Bofya kitufe cha End Call (Simu ya Kuhitimisha) ili uhitimishe ziara.**



  - **Ikiwa unahitaji kujiunga tena na ziara baada ya kuhitimisha simu, bofya kiungo kutoka kwenye barua pepe yako au ujumbe wa maandishi na uangalie tena. Hii inafanya kazi tu ndani ya dakika 5 baada ya kuhitimisha ziara.**


## Kutatua tatizo

- **Nina matatizo ya kamera au maikrofoni.**
  - **Hakikisha kuwa kivinjari chako cha intaneti kinaruhusiwa kufikia maikrofoni na kamera yako.**

1. **Fungua Settings (Mipangilio).**




2. **Sogeza chini hadi kwenye Apps (Programu).**




3. **Bofya app (programu) ya kivinjari cha intaneti unachotumia.**





4. **Bofya Camera (Kamera).**





5. **Hakikisha kwamba ruhusa zimewekwa kuwa Ask (Uliza) au Allow (Ruhusu).**




6. **Rudi na Ubofye Microphone (Maikrofoni).**





7. **Hakikisha kwamba ruhusa zimewekwa kuwa Ask (Uliza) au Allow (Ruhusu).**



Kujiunga na Miadi yako ya
KidCare Anywhere

Children's Mercy
KANSAS CITY

- Nimeshindwa kupata kiungo cha ziara yangu.
    - Kiungo kinatumwa kwenye barua pepe na simu yako mara 3 kabla ya ziara yako.
        - Wakati wa kuratibu
        - Saa 24 kabla
        - Dakika 15 kabla
    - Usishiriki kiungo hiki na wengine. Mtu 1 tu ndiye anayeweza kutumia kiungo hiki. Ikiwa wengine wanahitaji kujiunga kwenye ziara, mwambie mtoa huduma pindi ziara inapoanza.
    - Tafuta "Visitnow" katika ujumbe wa maandishi au barua pepe yako.
        - Hakikisha kuwa umeangalia folda zako za barua pepe Mbaya au Taka.




Kwa usaidizi wa kiufundi, piga simu (816) 302-7895

Ili kuratibu upya miadi yako, piga simu (816) 234-3700